
**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MJI MAFINGA**
**SHULE YA SEKONDARI ADONAI**
**S.L.P 275 MAFINGA-IRINGA**
**NAMBA YA USAJILI S.4651**
**SIMU: 0754610186, 0756704520,0655267111**
**Website: www.Adonaisecondary.ac.tz**




## MAELEZO NA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ADONAI KWA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2027

Ninafurahi kukuarifu kuwa mtoto wako amechaguliwa kujiunga na kidato cha Kwanza katika shule hii mwaka 2027. Shule ya sekondari Adonai ipo katika wilaya ya Mufindi (MAFINGA MJINI) kata ya Rungemba barabara kuu kilometa 15 kutoka Mafinga kuelekea Iringa

### 1. SIFA ZA KUJIUNGA NA SHULE

1) Awe amehitimu elimu ya msingi (darasa la saba 2026)
2) Awe amefanya na kufaulu mtihani wa shule ( interview examinations)
3) Akubaliane na masharti na sheria zote za shule

2. **ADA YA MASOMO KWA MWAKA**

Tunapenda kukujulisha kuwa ada ya masomo kwa mwanafunzi wa kkdato cha kwanza na wanaohamia ni Tzs 2,200,000/= Kwa wale wanaoendelea kidato cha pili, tatu na nne ada ni Tzs 2,000,000/=

**AWAMU ZA ULIPAJI WA ADA**

| NA | MUDA | KIDATO CHA KWANZA NA KUHAMIA TZS | KIDATO CHA PILI, TATU NA NNE |
|---|---|---|---|
| **1.** | **JANUARI-2026** | **1,000,000/=** | **800,000/=** |
| **2.** | **APRIL-2026** | **600,000/=** | **600,000/=** |
| **3.** | **JULY-2026** | **400,000/=** | **400,000/=** |
| **4.** | **SEPTEMBER-2026** | **200,000/=** | **200,000/=** |
| **5.** | **JUMLA KUU** | **2,200,000** | **2,000,000/=** |

3. **KUPITIA ADA HIYO MWANAO ATAPATA MAHITAJI YAFUATAYO KWA KIDATO CHA KWANZA NA WANAOHAMIA**

1. **Sare**

   WASICHANA

   - Sketi 3, shati 2, t-shirt 1, sweta 1

   WAVULANA

   - Suruali 3, shati 2, t-shirt 1, sweta 1

2. Godoro 01
3. Mashuka mawili 02

**MICHANGO MINGINEYO**

1 Gharama za matibabu kwa mwaka asiye na bima ni Tzs 20,000/= na kwa wale wenye bima ni Tzs 10,000/=

2 Tahadhari TZS 10,000/=

3 UMISETA TZS 2000/=

4 Mahafali TZS 20,000/=

**MAHITAJI YA PAMOJA**

1) Madaftari 12 makubwa (Counter books) Quire 3 au Zaidi.
2) KAMUSI (English/Swahili) kila mwanafunzi anatakiwa kuja na kamusi yake.
3) Rim 3 za karatasi nyeupe A4 kwa ajili ya kuchapishia mitihani
4) Fagio la chelewa lenye mpini mrefu (wote)
5) Chombo cha kulia chakula ( kikombe, kontena na kijiko)
6) Squizer (Mopper)
7) Jembe 1 lenye mpini
8) kwanja( fyekeo) kwa Wote
9) soksi nyeupe jozi 4 au zaidi (Wasichana), Walulana Soksi nyeusi jozi 4 au zaidi.
10) Viatu vya ngozi vyeusi jozi 2 visivyokuwa na kisigino kirefu wala kuchongoka mbele. Lazima viwe vya kufunga kwa kamba.
11) Track suit ya rangi nyeusi yenye mistari myeupe.
12) Kanda mbili( umoja) kwa ajili ya kuogea (Sio yeboyebo)
13) Ndoo moja (01) ndogo lita 10,kwa ajili ya kuogea
14) Vibanio vya nguo

**N.B kila mwanafunzi anatakiwa kuja na BIBLIA NA TENZI ZA ROHONI**

**5. AINA YA SHULE**

Shule yetu ni mchanganyiko inayowapokea wanafunzi wa kike na kiume katika mazingira salama na rafiki kwa wote na tunazingatia usawa, nidhamu, na maadili mema kwa kila mwanafunzi bila ubaguzi. Wanafunzi husoma pamoja huku wakijengewa uwezo wa kushirikiana na kuheshimiana

Pia shule inawalea watoto katika maadili na misingi ya kikristo yenye lengo la kumfannya mtoto amjue mungu

6. MASOMO YANAYOFUNDISHWA

1. Wanafunzi watasoma masomo yote ya Sanaa, sayansi na biashara pia walimu na wanafunzi wanakuwepo shuleni muda wote

- NB: MALIPO YOTE YA ADA NI LAZIMA YAFANYIKE BANK YA CRDB
- NAMBA YA AKAUNTI : 0150859860500
- JINA LA AKAUNTI :ADONAI SECONDARY SCHOOL
- PIA MICHANGO YOTE ILIPIWE SHULENI

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na- 25 ya mwaka 1978, na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya Elimu chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu.

**Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo**

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.

c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa

d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

e) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule

f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa

g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na

h) Kutunza mali ya shule

i) Mwanafunzi atakayeshindwa kupata wastani wa alama 50% katika mitihan yote na mazoezi yanayotolewa darasan kwa mwanafunzi hatafikisha wastani mzazi atalazimika kumtafutia shule nyingine

**A: Mahudhurio**

Kila mwanafunzi ni lazima aamke mapema na kufanya usafi wa mazingira na kuhudhuria gwaride la ukaguzi wa usafi na kuchangamsha mwili.

1. Mwanafunzi yeyote haruhusiwi kuondoka (Kutoroka) katika eneo la shule bila kupata kibali/ruhusa kutoka kwa mwalimu mkuu.
2. Siyo ruhusa kwa mwanafunzi kukosa kufika shuleni bila kupata kibali. Ruhusa itatolewa kwa sababu maalum tu na hata hivyo mzazi/mlezi analazimika kufika kuomba ruhusa na kujieleza kimaandishi.
3. Kila mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi vyote vya darasani na shughuli za michezo na uzalishaji mali atakavyotakiwa na ratiba bila kuchelewa.
4. Mwanafunzi ni lazima afanye mitihani na majaribio ya masomo yote anayosoma.

**B: Tabia na Mwenendo**

Kila mwanafunzi lazima awe na nidhamu ya hali ya juu kuwaheshimu wafanyakazi wote na wanajumuiya kwa jumla. Mwanafunzi asiye na nidhamu atapoteza nafasi yake.

1. Mwanafunzi haruhusiwi kufanya yafuatayo:
   a) Kuvaa Pete
   b) Kunyoa nyusi
   c) Kuvaa Hereni
   d) Kupaka Hina na Rangi za Kucha
   e) Kuwa na Kucha ndefu
   f) Kusuka nywele
   g) Kuweka dawa nywele.
   h) Kunyoa kipara au mitindo
   i) Kuvaa mlegezo wa Sketi au Suruali

j) Kuwa na ndevu

k) Kuvaa rozari au tasbihi

2. **Makosa yafuatayo yatapelekea mwanafunzi kuadhibiwa na kuonywa;**

a) Uchelewaji wa sehemu yoyote anapohitajika

b) Kutofanya kazi za usafi wa mazingira

c) Kutojali masomo na ratiba za shule

Aidha, Mwanafunzi anazo nafasi mbili tu za kuonywa na baada ya hapo kikao kinachohusika kitamchukulia hatua kali zaidi.

**C:** **Makosa yanayoweza kumfukuzisha/kumsimamisha mwanafunzi bila** ya kuonywa

a) Wizi

b) Uasherati na ushoga

c) Ubakaji

d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile Bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k e) Kupigana au kupiga na kutumia lugha za matusi

f) Kuharibu kwa makusudi mali ya shule

g) Kudharau bendera ya Taifa

h) Kuwa mjamzito/kupata mimba au kusababisha ujauzito

i) Kuoa au kuolewa

j) Kutoa mimba

k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu

l) Dharau,ukaidi,ubishi,utoro,uvivu,upigaji kelele,kukaa maeneo yasiyoruhusiwa na kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa

m) Kukataa adhabu kwa makusudi.

n) Kuvaa nguo za nyumban au zisizo sare ya shule

o) Kuwa na simu ya mkononi shuleni

**D:Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni wakati wa usajili.**

a) Fomu ya Mzazi/Mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na taratibu za shule pamoja na maelekezo mengine yatakayotolewa shuleni. ( ***Fomu A***)

b) **Medical Examination form** ambayo itajazwa na Hospitali ya Serikali, aidha fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni kabla ya kuanza muhula wa masomo.(***Fomu B)***

**FOMU A**

**SHULE YA SEKONDARI ADONAI**

**FOMU YA KUANDIKISHWA SHULENI**

**A. TAARIFA ZA MWANAFUNZI (ijazwe na mwanafunzi)**

| PICHA YA MWANAFUNZI |
|---|

Jina kamili la mwanafunzi…………………………………………………...

Tarehe ya kuzaliwa ……………………………………………………….

Mahali alipozaliwa ………………………………………….

( wilaya/Mkoa)
Taifa……………………………………………………………………….

Uraia ……………………………………………………………………….

Saini ya mwanafunzi ……………….…… Tarehe ……………….…

**B: TAARIFA YA MZAZI/MLEZI (Ijazwe na Mzazi/Mlezi)**

| PICHA YA MZAZI/MLEZI |
|---|

Jina kamili la Mzazi/Mlezi ……………….………………………..……………………………

Utaifa …………………………..………………………………………

Uraia ………………………………..……………………………….

Anuani ya ………………………..……………………………….….

Sehemu unayoishi ………………………..…………………….…….

Mtaa …………………………………….……………………….……..

Mkononi ……………………………………….……(Ikibadilika toa taarifa)

Eleza kama mtoto ana matatizo yoyote ya kiafya ……………………………………..
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………...………………………………..

Saini ya Mzazi/Mlezi ………………………… Tarehe……………………

**FORM B**

## MEDICAL EXAMINATION

To be completed by medical officer from an government hospital

Full name student full name ……………………………………… Age: …………… Years. Sex ……………….

Blood Count (Red and White)…………………………… Stool Examination ………………………………………..

Urine analysis ……………………………………………. Syphilis Test ……………………………………………..

EyeTest………………………………………, T.B Test ………………………Ears …………………………

Chest…………………………………………. Spleen…………………………………………….

Abdomen ………………………………………………….

B: Recommend if the student is fit for studentship (i) Yes (ii) No

……………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………

C: Any other advice

……………………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

Name, Designation and Signature Date ………………… Stamp………………

**FOMU C**

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA AHADI

MKUU WA SHULE,

SHULE YA SEKONDARI ADONAI

S.L.P 275,

MAFINGA-IRINGA.

**TAMKO LA MWANAFUNZI**

Mimi (Mwanafunzi) jina kamili …………………………………………………………………

Ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha ……………........
Mwaka…………………………… katika Shule ya Sekondari Adonai

Ninaahidi kwamba: Nitatii sheria zote za shule kama nilivyozisoma

Nitaweka bidii katika masomo, kazi na shughuli zote za kishule. Nitashiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji mali, kuzalisha mali iliyo bora bila kushurutishwa. Sitaitia hasara shule kwa kuharibu au kupoteza malighafi (raw materials)

Nitakuwa mwanafunzi mwenye nidhamu ya hali ya juu, mkakamavu na mwenye mwenendo safi wakati wote hata nikiwa nje ya shule kwa madhumuni ya kuipa na kutunza sifa ya shule ya sekondari Adonai

Saini ya Mwanafunzi …………………..……………. Tarehe …………………………

**TAMKO LA MZAZI/MLEZI**

Mimi ( Jina kamili la Mzazi/Mlezi) …………………………………………………………….

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………………………………………………………………..

**Naahidi kwamba**

1 Nitampatia mtoto wangu mahitaji yote muhimu ya shule kama yalivyoelezwa katika maelekezo ya kujiunga na shule
2 Nitakua tayari kutoa msaada wowote utakaohitajika (maoni,adhabu n.k) katika kumlea mtoto wangu
3 Nitamhimiza mtoto wangu kusoma kwa bidii, kufanya mazoezi ya masomo yake (Home work) na kufuatilia maendeleo na tabia yake shuleni.
4 Mtoto wangu akiwa nyumbani nitamlea katika maadili mema anayostahili ili awe mfano mzuri shuleni na katika jamii kwa ujumla.
5 Nitalipa ada kwa awamu zilizopangwa nakuonesha ushirikiano na uongozi wa shule.

Saini ya Mlezi/Mzazi …………………..………… Tarehe ………………………………